Arafa ya sera

Nambari 33 Juni 2013

Taasisi zilizoshirikiana: Wizara ya Afya ya Umma na Usafi na Taasisi ya Kumbukumbu za Idadi ya Watu (PRB)

Changamoto za Idadi ya Watu, Afya na Mazingira: Ni Nini Serikali za Kaunti Zinaweza Kufanya?

Chini ya Katiba mpya ya Kenya, serikali za kaunti ndizo zitakazosimamia kaunti zote 47 zilizobuniwa kufikia mwezi Machi 2013. Kwa ushirikiano wa mabaraza ya kaunti, magavana na maafisa wakuu wa serikali hizo watapanga, kutayarisha bajeti na kutekeleza miradi ya maendeleo. Miradi hiyo itakuwa na faida kubwa zaidi endapo masuala ya idadi ya watu, afya na mazingira yatatiliwa maanani wakati wa kupanga na kutayarisha za miradi hiyo.

Arafa hii ya sera inaangazia jinsi ya kushughulikia masuala ya idadi ya watu, afya na mazingira (PHE) ili kuboresha maisha ya wakenya na kuliwezesha taifa hili kusalia katika njia ya kuafikia malengo ya ruwaza ya maendeleo ya mwaka 2030.

Mienendo Kuhusu Idadi ya Watu na Sera Nchini Kenya

Wakati Kenya ilipojinyakulia Uhuru mwaka wa 1963, idadi ya watu ilikuwa takriban milioni 9 jinsi inavyoonyeshwa katika mchoro nambari 1. Miaka hamsini baadaye idadi hiyo imeongezeka zaidi ya mara nne na kufikia watu milioni 38.6 (kwa mujibu wa matokeo ya hesabu ya watu ya mwaka 2009), na idadi hiyo inazidi kuongezeka kwa watu milioni moja kila mwaka.[1] Ongezeko hili la watu limekuwa changamoto kubwa kwa uchumi wa taifa hili na rasilimali zake. Endapo hali hii itaendelea, taifa hili litakuwa na takriban watu milioni 70 ifikapo mwaka 2050.

Mchoro 1: Ongezeko la Idadi ya Watu Nchini Kenya 1962-2009



Kutoka: Taasisi ya Kitaifa ya Takwimu Nchini Kenya, Hesabu ya watu nchini Kenya (1962, 1969, 1979, 1989, 1999, 2009)

Idadi ya watu wanaoishi katika maeneo ya mijini hapa nchini iliongezeka kutoka asilimia 7.8 mwaka wa 1962 hadi asilimia 32 mwaka 2012, hususan baada ya vijana wengi kuhamia mijini kutafuta ajira.[2]

Idadi ya watu wanaoishi mijini inatarajiwa kuwa zaidi ya nusu ya idadi ya watu wote hapa nchini ifikapo mwaka 2050.[3] Kutokana na hayo, mahitaji ya nyumba, maji, huduma za elimu na afya yameongezeka huku mazingira katika maeneo ya miji yakizidi kuzorota kwa sababu ya msongamano wa watu na kuchipuka kwa mitaa ya mabanda.[4] Wakati huo huo idadi kubwa ya Wakenya bado wanaishi katika sehemu za mashambani ambako wanakabiliwa na changamoto za aina yake, mbali na zile zinazowakabili wakaazi wa mijini.

Serikali imekuwa ikibuni mikakati ya kuhakikisha ongezeko la idadi ya watu halipiku rasilimali zilizoko hapa nchini. Mpango wa kitaifa wa upangaji uzazi ulianzishwa mwaka 1967 na kufuatiwa na kubuniwa kwa Baraza la Kitaifa kuhusu Idadi ya watu na Maendeleo (NCPD) katika miaka ya themanini pamoja na kutolewa kwa mwongozo wa sera kuhusu idadi ya watu (1984). Mnamo mwaka 2000, serikali ilibuni sera madhubuti kuhusu idadi ya watu iliyojulikana kama Sera ya Kitaifa kuhusu Idadi ya Watu na Maendeleo endelevu. Mnamo mwaka wa 2012 serikali ilibuni sera kuhusu idadi ya watu na ustawi wa kitaifa. Sera hizi zimesaidia kuimarisha matarajio ya idadi ya watu na afya. Kwa mfano idadi ya watoto wanaozaliwa na mwanamke ilipungua kutoka 8 mnamo miaka ya 1970 hadi watoto 5 mnamo 2010.[5] Hata hivyo hatua zaidi zinahitaji kuchukuliwa ili kudhibiti kasi ya ongezeko la idadi ya watu kuweza kupunguza mzigo wake kwa rasilimali za kitaifa na kuboresha maisha ya Wakenya.

Jukumu la serikali za kaunti katika maendeleo

Katiba ya Kenya inazipatia serikali za kaunti jukumu muhimu la kuimarisha ustawi na hali ya maisha nyanjani. Baadhi ya majukumu ya serikali hizo ni; Kuboresha miradi ya kilimo, Kutoa huduma za afya ya jamii, Kusimamia miradi ya kuhifadhi mazingira, Kudhibiti matumizi ya ardhi, Kutoa huduma za maji na usafi na Kukomesha uchafuzi wa mazingira. Ili kutekeleza majukumu hayo serikali za kaunti zimepewa uwezo wa kisheria na udhibiti na zinatarajiwa kuhakikisha umma unashirikishwa katika maswala yote ya maendeleo. Mfumo wa sheria ukijumuishwa na fedha zinazotengewa serikali hizo kila mwaka unatoa nafasi muhimu kwa serikali za kaunti kushughulikia kikamilifu changamoto za idadi ya watu, afya na mazingira (PHE) kama mojawapo ya mipango ya maendeleo.

Changamoto kuhusu idadi ya watu, afya na mazingira zina uhusiano

Mazingira na Mbinu za Kujikimu Kimaisha

Jamii nchini Kenya zinategemea mali ghafi kama vile ardhi kwa ujenzi na kilimo, chakula cha nyumbani na viwandani na makaa na kuni vinavyotumika kama kawi. Mabadiliko ya mazingira pamoja na ongezeko la kasi la idadi ya watu yamesababisha kufyekwa kwa misitu katika maeneo makubwa ya ardhi ili kutoa nafasi kwa ujenzi wa makazi na shughuli za kilimo, kukatwa kwa miti inayotumiwa kama kawi pamoja na upungufu wa maji. Uharibifu wa misitu hapa nchini umesababisha kuharibiwa kwa mazingira na maji ya mvua. Hali hii imesababisha mmomonyoko wa udongo katika maeneo mengi hapa nchini pamoja na uchafuzi na kuharibiwa kwa vyanzo vya maji. Mmomonyoko wa udongo umepunguza uwezo wa taifa hili kuzalisha chakula na hivyo kusababisha baa la njaa la mara kwa mara na mizozo ya kijamii.[6] Uchafuzi wa vyanzo vya maji unaosababishwa na udongo, mbolea na dawa za kuua wadudu umechangia pakubwa mfumuko wa maradhi mbalimbali.[7]

Mchoro wa 2 unaonyesha kwamba asilimia 82 ya familia za humu nchini hutegemea makaa au kuni kama kawi ya kupikia, hivyo kupunguza kiwango cha eneo la msitu hapa nchini. Kwa sasa ni asilimia 3 tu ya ardhi ya Kenya ambayo iko chini ya misitu, kiwango ambacho ni cha chini sana ikilinganishwa na kiwango kilichopendekezwa kimataifa cha asilimia 10. Kuongeza kiwango cha eneo la msitu hapa nchini kutapunguza mmomonyoko wa udongo, kukomesha kuenea kwa jangwa, kuimarisha akiba ya chakula, kuhifadhi chemi chemi za maji, kuongeza idadi ya wanyama pori na bidhaa za misitu. Hatua zinazoweza kuchukuliwa ili kuongeza na kuhifadhi misitu ni pamoja na kubuni vyanzo mbadala vya kawi ya kutumiwa nyumbani kama vile majiko ya kuokoa kawi ambayo hutumia makaa au kuni chache na matumizi ya majiko yanayotumia kinyesi cha wanyama.

Kujitosheleza kwa chakula au kupata chakula kwa urahisi ni muhimu kwa afya na maisha ya watu. Hata hivyo uwezo wa kuzalisha chakula cha kutosha unakabiliwa na

Mchoro2: Asilimia ya kutanda kwa familia kwa kuzingatia aina ya kawi ya kupikia



Kutoka: Taasisi ya Kitaifa ya Takwimu Nchini Kenya na ICF International, Utafiti wa Hali ya watu kimaeneo na Afya nchini Kenya 2008-9 (KDHS).

changamoto nyingi kutokana na uharibifu wa mazingira na ung'ang'aniaji maji na kawi jinsi inavyodhihirishwa na ongezeko la visa vya njaa na magonjwa ya utapiamlo.[8]

Wakenya wengi wanategemea uvuvi na kilimo kujipatia riziki. Kwa sasa takriban familia milioni 5 zinajihusisha na shughuli za kilimo lakini mabadiliko ya mazingira pamoja na mifumo duni ya kilimo yanasababisha vikwazo vya kujikimu kimaisha kutokana na shughuli za kilimo. Vivyo hivyo jinsi idadi ya watu inavyizidi kuongezeka ndivyo mashamba yanavyoendelea kugawanyiwa jamaa na hivyo kuwa madogo zaidi na kupungua manufaa ya kuzalisha chakula cha kutosheleza jamii au kuuzwa kwa ajili ya mapato.

Sekta ya uvuvi inahusisha wavuvi wapatao 60,000 na zaidi ya watu nusu milioni wanaotengemea moja kwa moja bidhaa zinazotokana na samaki pamoja na biashara ya utayarishaji bidhaa za samaki.[9] Hata hivyo mbinu zisizofaa za uvuvi na uvuaji samaki kupita kiasi vimesababisha kupungua kwa idadi ya samaki wanaopatikana kwenye maziwa kila mwaka na hivyo kupunguza uwezo wa kujitegemea kwa chakula na mapato yanayotokana na shughuli hiyo.

Ili Kenya iweze kuimarisha hali ya maisha ya wananchi, mbinu hizi za kujipatia riziki lazima zilindwe.

Idadi kubwa ya wanyama pori nchini Kenya inaendelea kuiletea serikali mapato kupitia sekta ya utalii ambayo inachangia asilimia 10 ya jumla ya pato la kitaifa kila mwaka. Hata hivyo katika miaka ya hivi majuzi mizozo kati ya binadamu na wanyama pori imezidi kushuhudiwa kutokana na ongezeko la mahitaji ya ardhi na malighafi nyingine.

Mara nyingi mizozo hii husababishwa na watu wanaojenga makazi au kulima kwenye malisho ya wanyama pori au wanyama pori kuvamia mashamba wakitafuta malisho. Hivyo serikali ina jukumu la kuhakikisha binadamu na wanyama pori wamelindwa.

Wanawake

Wanawake nchini Kenya wanaathiriwa pakubwa na mazingira duni na ukosefu wa mbinu mbadala za

kujikimu maishani. Kwa kiasi kikubwa hali hii inatokana na majukumu mengi ya nyumbani yanayowasonga. Baadhi ya majukumu hayo ni kulea watoto, kutafuta kuni, kupanda mimea ya chakula, kupika na kuwatunza wagonjwa katika familia. Wanawake huumia zaidi kutokana na uharibufu wa mazingira kwani hudhoofika kiafya, kuwa fukara, kukosa kuni na malighafi nyingine, maswala yanayowiana na majukumu ya wanawake.

Changamoto kubwa inayowakabili kina mama ni kutokuwa na uwezo wa kupanga au kuamua wakati wa kushika mimba na ni mara ngapi watapata watoto. Kuwasaidia waliooana kupanga idadi ya watoto wanaotaka kunaweza kuboresha afya ya wanawake na watoto na kupunguza mzigo mkubwa wa kiuchumi katika familia na mzigo kwa matumizi ya malighafi.

Mchoro nambari 3 unaonyesha kwamba miongoni mwa wanawake walio na umri wa chini ya miaka 20 na wale walio kati ya miaka 35 na 39, takriban nusu ya watoto wanaozaliwa ni wale ambao hawakutarajiwa. Kwa wanawake walio na umri wa kati ya miaka 21 na 34 zaidi ya thuluthi moja ya watoto wanaozaliwa hawakutarajiwa. Hali kadhalika thuluthi mbili ya watoto wanaozaliwa na wanawake walio na umri wa kati ya miaka 40 na 44 hawakutarajiwa.

Idadi kubwa ya watoto wanaozaliwa ambao hawakutarajiwa inatokana na ukweli kwamba idadi kubwa ya wanawake ambao hawataki kushika mimba hawatumii dawa za kupanga uzazi. Wanawake hawa wana hitaji fulani ambalo halijatimizwa kwa kupanga uzazi.

Mchoro 3: Asilimia ya kutanda kwa Uzazi bila Mpango miongoni mwa wanawake wanaijifungua kwa kuzingatiwa umri



Kutoka: Taasisi ya Kitaifa ya Takwimu Nchini Kenya na ICF International, Utafiti wa Hali ya watu kimaeneo na Afya nchini Kenya 2008-9 (KDHS).

Miongoni mwa wanawake walioolewa nchini Kenya, asilimia 46 wanatumia dawa za kupanga uzazi, ilihali asilimia 26 hawatumii dawa hizo. Kushughulikia hitaji hili la upangaji uzazi ambalo halijatekelezwa kwa kuongeza uwezekano wa wanawake hao kupata dawa za kupanga uzazi ni fursa muhimu ya kuimarisha maisha ya wanawake na kulinda jamii.....

Kuwawezesha wanawake kupata kwa urahisi huduma za afya wanazozihitaji pia ni njia moja ya kuwasilisha ujumbe kuhusu mazingira kwao.

Afya: maji na usafi

Maradhi ya kuendesha yanaendelea kusababisha vifo vingi na kuugua miongoni mwa watoto walio na umri wa chini ya miaka-5. Kwa mujibu wa ripoti ya KDHS ya mwaka 2008-09, mmoja kati ya watoto watano hapa nchini huugua kutokana na tatizo la kuendesha mara kwa mara. Maswala ya mazingira yakiwemo maji machafu na ukosefu wa usafi ni chanzo kikuu cha maradhi hayo miongoni mwa watoto wengi. Kupatikana kwa maji safi na vifaa vya usafi kunaathiriwa na ongezeko la idadi ya watu. Endapo idadi ya watu itaongezeka kwa kasi zaidi kuliko ongezeko la vifaa vya usafi basi vifaa hivyo haviwezi kutimiza mahitaji ya watu na hivyo kusababisha mfumko wa maradhi.

Hali hii inashuhudiwa katika mitaa mingi ya mabanda katika maeneo ya miji hapa nchini.

Mchoro nambari 4 unaashiria kwamba familia mbili kati ya tatu hapa nchini zinaweza kupata maji safi kama vile maji ya mfereji, chanzo cha maji kilichohifadhiwa au kisima. Kwa jumla katika maeneo ya miji, 9 kati ya nyumba 10 zinapata maji safi ikilinganishwa na nyumba 5 kati ya 10 katika maeneo ya mashambani.

Mchoro 4: Asilimia ya kutanda kwa familia kwa kuzingatia viashirio vya usafi na mahali wanakoishi



Kutoka: Taasisi ya Kitaifa ya Takwimu Nchini Kenya na ICF International, Utafiti wa Hali ya watu kimaeneo na Afya nchini Kenya 2008-9 (KDHS).

Aidha mchoro huo unaonyesha kwamba chini ya nusu ya familia zote hapa nchini hutumia mbinu mwafaka za kusafisha maji ili kuyafanya safi kwa matumizi ya nyumbani.

Matumizi ya vyoo halisi kama vile vyoo vya kisasa vilivyounganishwa na mabomba ya majitaka, shimo la kuondoa taka au choo kilichochimbwa na kujengwa vizuri vinapatikana katika asilimia 23 ya nyumba kote nchini. Katika maeneo ya mijini ambako inatarajiwa kuwe na vyoo vingi zaidi, ni asilimia 30 tu ya familia ambazo zina vyoo hivyo. Katika ameneo ya mashambani, nyumba moja kati ya tano zina vyoo bora. Hivyo maji na vifaa vya usafi lazima viimarishwe ili kupunguza maambukizi ya maradhi ya kuendesha.

Mbinu ya idadi ya watu, afya na mazingira (PHE)

Mbinu ya "PHE" inaangazia uhusiano tata kati ya binadamu, afya yao na mazingira. Inahimiza matumizi ya mikakati jumuishi ili kuimarisha uwezo wa kupata

NCPD ni shirika la Serikali linalobuni na kuimarisha sera za idadi ya watu na kushirikisha shughuli zinahusiana kwa ustawi wa maendeleo nchini Kenya.

NCPD

Shirika la Kitaifa la Ushirikishi wa Idadi ya Watu na Maendeleo

S.L.P. 48994 - GPO, Nairobi 00100, Kenya

Simu: 254-20-271-1600/01

Kipepesi 254-20-271-6508

Baruapepe:info@ncpd-ke.org

www.ncpd-ke.org

USAID | KENYA
FROM THE AMERICAN PEOPLE

IDEA INFORMING DECISIONMAKERS TO ACT

PRB INFORM EMPOWER ADVANCE

Jarida hili limechapishwa kwa Ushirikiano wa Watu wa Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya kimataifa (USAID) chini ya Mradi wa IDEA (No. AID-0AA-A-10-00009). Yaliyomo kwenye jarida hili yamekusanywa na Shirika la Kitaifa la Ushirikishi wa Idadi ya Watu na Maendeleo (NCPD) na hayaangazii maoni ya Shirika la USAID wala Serikali ya Marekani.

huduma za afya hususan dawa za kupanga uzazi na afya ya uzazi huku ikisaidia jamii kusimamia na kutunza mazingira wanayotegemea katika maisha yao.

Faida ya mikakati jumuishi ya PHE ni kwamba inaweza kufikia jamii zinaoishi katika maeneo yasiyofikika kwa urahisi, kushughulikia maswala nyeti ya kijamii ambayo mara kwa mara hutangamana, kupunguza uharibifu na kuimarisha ushiriki wa wanawake na wanaume katika miradi ya maendeleo.

Mifano ya miradi jumuishi ya PHE ni ile inayozungumzia upangaji uzazi na uhifadhi wa mazingira; magonjwa ya kuambukizana na uhifadhi wa maji pamoja na upangaji uzazi na kujitosheleza kwa chakula.

Mapendekezo

Ili serikali za kaunti zifaulu kushughulikia kikamilifu maswala ya PHE kwanza kabisa lazima zibuni miundo itakayotambua, kupanga na kutekeleza miradi ya PHE. Kuambatana na hayo Baraza la Kitaifa kuhusu Idadi ya Watu na Maendeleo linapendekeza serikali za kaunti zizindue miradi ifuatayo katika kila kaunti:

- Kuimarisha ushirikiano wa taasisi husika katika miradi mbalimbali. Ushirikiano huu utabuni jopo la PHE katika kila kaunti. Mshirikishi wa idadi ya watu katika kila kaunti atatekeleza ajenda hii katika mwaka wa kwanza tangu kutekelezwa kwa mfumo wa serikali za kaunti na kila mwaka atahakikisha kwamba washirika hao wanaendelea kufanya kazi pamoja kupitia jopo la PHE.
- Kujumuisha changamoto, mbinu na malengo ya PHE kwenye mikakati ya maendeleo ya kaunti. Mshirikishi wa idadi ya watu kwenye kaunti ataongoza utekelezaji wa mfumo huo kwa ushirikiano na wenzake kwenye jopo la PHE. Haya yanaweza kutekelezwa wakati mipango ya kaunti inapobuniwa ili kuhakikisha miradi ya maendeleo inashughulikia ajenda za PHE.
- Husisha jamii katika kutambua mahitaji ya PHE katika mwaka wa kwanza wa kuwepo kwa serikali ya kaunti. Mshirikishi wa maswala ya idadi ya watu atatoa mwongozo kwa wadau kuhusu mfumo huu ambao hatimaye utahusisha upangaji na utekelezaji wa miradi jumuishi ya PHE ambayo inashughulikia mahitaji husika.
- Kujifunza kutokana na miradi ya PHE iliyofaulu. Wafanyikazi kutoka angalau mradi mmoja wanaweza kutembelea kaunti nyingine kila mwaka kutathmini ufanisi wao. Hili litawasaidia washika dau kuimarisha upangaji na utekelezaji wa miradi yao. Mifano ya miradi hiyo ni kama vile:
- Afya ya watu na mazingira- eneo la Ziwa Victoria (HoPE LVB) mjini Kisumu, shirika la Greenbelt Movement na lile la Family Health International, pamoja na mradi wa kuhifadhi wanyama wa majini unaodhaminiwa na shirika la wanyama pori ulimwenguni katika eneo la Kiunga. Hali kadhalika washirika wa jopo la PHE wanaweza kuzuru miradi mingine iliyofaulu.
- Kutambulisha na kusambaza desturi bora katika kaunti kila mwaka ili kutoa fursa kwa jamii kupata mafunzo yanayoweza kutumika mahali pengine. Jopo la PHE litakuwa na jukumu la kutekeleza pendekezo hili.
- Kubuni takwimu za viashirio muhimu vitakavyotumiwa kukagua na kutathmini miradi yote ya PHE kwenye kaunti. Taasisi ya kitaifa ya takwimu kwenye kaunti ikishirikiana na washika dau wengine itakuwa na wajibu wa kutekeleza pendekezo hili ambalo linapaswa kutekelezwa katika mwaka wa kwanza wa kuwepo kwa serikali ya kaunti.

Hitimisho

Kaunti mpya zilizobuniwa zinatofautiana kwa idadi ya watu na matabaka, afya na mazingira lakini zote zinakabiliwa na changamoto zinazoshabihiana za idadi ya watu, afya na mazingira. Kaunti hizo sasa zina nafasi ya kushughulikia changamoto hizo zinazohusiana kwa kubuni miradi iliyopendekezwa hapo juu ambayo itaweka msingi wa kutekeleza miradi ya PHE itakayoshughulikia mahitaji ya maendeleo nyanjani. Kushughulikia maswala ya idadi ya watu, afya na mazingira kupitia mbinu jumuishi kunaweza kupunguza uharibifu wa mazingira, umaskini na ukosefu wa chakula pamoja na kuimarisha afya ya wakenya.

Kumbukumbu

[1] Kenya National Bureau of Statistics (KNBS), *Kenya Population and Housing Census – 1999* (Nairobi: KNBS, 2010).

[2] W.T.W. Morgan, "Urbanization in Kenya: Origins and Trends," *Transactions of the Institute of British Geographers* No. 46 (United Kingdom: Wiley, 1969).

[3] Population Reference Bureau (PRB), 2012 *World Population Data Sheet* (Washington DC: PRB, 2012).

[4] W.L Riley et al., "Slum health: Diseases of Neglected Populations," *BMC International Health and Human Rights*, London, United Kingdom, 2007).

[5] National Council for Population and Development (NCPD), *Sessional Paper No. 3 of 2012 on Population Policy for National Development* (Nairobi: NCPD, 2012).

[6] C.I. Lang, *Environmental Degradation in Kenya as a Cause of Political Conflict, Social Stress, and Ethnic Tensions* (Zurich, Switzerland: Centre for Security Studies, 1995).

[7] H. Mogaka et al., "Climate Variability and Water Resources Degradation in Kenya: Improving Water Resources Development and Management," *World Bank Working Paper* No. 69 (Washington DC: World Bank, 2006).

[8] P.R. Ehrlich et al., "Food Security, Population, and Environment," *Population and Development Review* Vol. 19 (Washington DC: Population Council, 1993).

[9] Government of Kenya, *Kenya Vision 2030: A Globally Competitive and Prosperous Kenya* (Nairobi: 2007).

© 2013 Shirika la Kitaifa la Ushirikishi wa Idadi ya Watu na Maendeleo (NCPD)